




# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



## JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.34. Msimu wa Kilimo 2022/23

Tathmini ya September 1-10, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Septemba 11-20, 2023

### MUHTASARI

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini zinatarajiwa kuongeza unyevunyevu katika udongo.
- Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Vuli wanashauriwa kuendelea na maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu wa kilimo unaotegemea mvua za Vuli.


### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2023

**K** ipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi katika maeneo yaliyopo kaskazini mwa nchi (hususan katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria).

Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la juu kidogo ya wastani wakati lile la eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii iliendelea kuwa na mchango katika kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani.

### TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2023

**K** atika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu, wakati baadhi ya maeneo yalipata mvua kiasi cha chini ya milimita 25 katika siku 10 husika. Ni maeneo machache tu yaliyopata zaidi ya milimita 150 za mvua, kama inavyoonekana katika Kielelezo.



Kielelezo: Kiasi cha mvua cha Septemba 1-10, 2023 kama kilivyokadiriwa na satellite (RFE)

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2023

**K** atika dikadi hii baadhi ya maeneo nchini yalikuwa makavu kwa ujumla. Hali hii iliathiri upatikanaji wa maji lakini pia ilisaidia katika shughuli za uandaaji wa mashamba.

Kwa maeneo yanayopata mvua za vuli, wakulima waliendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya msimu wa kilimo wa mvua za vuli.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ulipungua kutokana na hali ya ukavu inayoendelea.

**HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA  
SEPTEMBER 1-10, 2023**

**K**wa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji

kwenye mito vimeendelea kupungua katika mabonde mengi nchini kutokana hali ya ukavu inayoendelea.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA  
KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20 2023**

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu kidogo wakati ile iliyopo kaskazini inatarajiwa kuimarika kidogo. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi katika maeneo yaliyopo kaskazini mwa nchi hususan maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi na kuimarisha mifumo isababishayo mvua.

Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani, hali hii inatarajiwa kuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani hususan katika nusu ya kwanza ya dekada.

Joto la bahari katika eneo la kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, hivyo kuwa na mchango hafifu katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi

**HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA  
KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2023**

**M**aeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) kunatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa hususan katika nusu ya kwanza ya dekada.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla, hata hivyo maeneo machache yanatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua nyepesi.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa mkoa wa Morogoro) inatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

**HALI YA HEWA KILIMO:  
MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA  
SEPTEMBER 1-10, 2023**

**H**ali ya mvua inayotarajiwa hususan katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi zitasaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Vuli wanashauriwa kuendelea na shughuli za kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa kilimo unaotegemea mvua za vuli.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi kutokana na hali ya upepo inayojitokeza mara kwa mara.

Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini, wafugaji wanashauriwa kutumia maji na malisho yaliyopo kwa uangalifu.

**HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA  
KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2023**

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi. Jamii inashauriwa kuendelea kutumia maji yaliyopo kwa uangalifu kufuatia kuendelea kwa msimu wa ukavu katika maeneo mengi nchini.